**HOTUBA YA MHESHIMIWA IAKAYA MRISHO KIKWETE,**
**RAIS WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA,**
**KWENYE UZINDUZI WA CHUO KIKUU KISHIRIKI CHA USHIRIKA**
**NA STADI ZA BIASHARA, MOSHI**
**(TAREHE 18 MACHI 2006)**

Mheshimiwa Waziri wa Elimu ya Juu, Sayansi na Teknolojia;

Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika;

Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro;

Mheshimiwa Mkuu wa Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine;

Wageni waalikwa;

Mabibi na Mabwana.

Awali ya yote, napenda nichukue fursa hii kutoa shukrani zangu za dhati kwa Uongozi wa Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine na Chuo Kikuu Kishiriki cha Ushirika na Stadi za Biashara-Moshi, kwa kunialika kushiriki nanyi katika uzinduzi wa Chuo hiki. Nawashukuru kwa mapokezi mazuri. Nawashukuru pia kwa burudani ya nyimbo nzuri.

Ndugu Mwenyekiti,

Leo ni siku kubwa na muhimu kwa sekta mbili kubwa na muhimu kwa maendeleo ya Taifa letu: Sekta ya Elimu ya Juu na Sekta ya Ushirika. Tunatimiza ahadi na wajibu wetu wa kuongeza nafasi za Elimu ya Juu kwa vijana wetu na Watanzania kwa ujumla. Vilevile, tunaongeza ujuzi, maarifa na uwezo wa uendeshaji wa Ushirika, ambao ni nguzo muhimu ya vanyonge kuondokana na umaskini.

Nawashukuru kwa kunipa fursa hii adimıu na ya kihistoria ya kuzindua Chuo Kikuu Kishiriki cha Ushirika na Stadi za Biashara. Nakushukuru sana Waziri wa Elimu ya Juu, Sayansi na Teknolojia kwa kunifanya nami niwe sehemu ya historia hii inayoandikwa hapa siku ya leo. Nawapongeza sana wale wote walioshiriki kuwezesha kuanzishwa kwa Chuo Kikuu hiki. Nawashukuru sana wafadhili ambao kwa kiasi kikubwa wamechangia kufikiwa kwa hatua hii. Wafadhili hao si wengi bali ni rafiki zetu wa Serikali ya Sweden na Shirika la SCC la nchi hiyo; Norway kupitia NORAD; Denmark kupitia DANIDA; Canada kupitia CIDA na DID; na Uholanzi kupitia SNV na NOVIB. Wengine ni Serikali za Marekanj Finland, Ufaransa, na Ujerumani. Kadhalika napenda kutambua mchango na msaada muhimu wa Shirika la Umoja wa Mataifa la Chakula na Kilimo Duniani (FAO); na Shirika la InWent la Ujerumani. Tunawaomba waendelee kukisaidia Chuo hiki kwani şaşa kina majukumu makubwa zaidi. Hakuna chuo kingine cho

chote Tanzania, au hata Afrika, kinachotoa elimu hii adimu kwa kiwango cha Shahada ya Chuo Kikuu. Hivyo basi, kusaidia Chuo hiki ni sawa na kusaidia Bara la Afrika.

Ndugu Mwenyekiti,

Wakati huu wa uzinduzi wa Chuo Kikuu Kishiriki hiki, ni muhimu kutafakari juu ya changamoto zilizo mbele yetu katika muktadha wa sekta ya Elimu ya Juu na ya maendeleo ya Ushirika hapa nchini. Kwa hiyo, naomba nitumie fursa hii kusema machache kuhusu siku ya leo na elimu ya juu kwa jumla.

Nilipotembelea Wizara ya Elimu ya Juu, Sayansi na Teknolojia katika utaratibu niliojiwekea wa kuternbelea Wizara za Serikali yetu, nilielezea hofu yangu juu ya harnu kubwa iliyopo kwa baadhi yetu kutaka kubadilisha kila taasisi ya mafunzo ya kati kuwa Chuo Kikuu. Hofu yangu ni kwamba tunaweza kufika mahali ambapo tuna wataalamu wa shahada wengi kuliko wataalamu wa kada ya kati na chini ya hapo ambao nao ni muhimu vilevile. Wataalamu wenye shahada wanawahitaji wataalamu wa kada hiyo ndipo wafanye kazi zao vizuri.

Hofu yangu hiyo ilikihusu pia Chuo Kikuu hiki tunachokizundua leo. Kama tujuavyo Chuo cha Ushirika Moshi kilikuwa na hili jukumu muhimu la kutengeneza kada ya kati ya wataalam wa ushirika na biashara nchini. Tena kimekuwa kinafanya hivyo kwa nchi kadhaa barani Afrika. Maelezo yenu yamenitoa hofu yangu. Nimefurahi sana kusikia kwamba pamoja na kuarnua kuwa Chuo Kikuu, bado mtaendelea kufundisha kada za kati kwa kutoa vyeti, stashahada na mafunzo mengine ya muda mfupi. Uamuzi huu ni wa busara na nawapongeeza sana. Mmeimaliza hofu niliyokuwa nayo niliposikia Chuo cha Ushirika Moshi kinageuzwa na kuwa Chuo Kikuu.

Ndugu Mwenyekiti,

Nimefarijika sana kusikia kwamba katika Chuo Kikuu hiki kipya, licha ya kuwapata wataalamu mahiri katika masuala ya ushirika, tutaendelea pia kuwapata Mabwana Ushirika. Umuhimu wa kada hii hauna haja ya kusisitizwa. Mabwana Ushirika ndio watu ambao wapo karibu na wananchi na ndio wanaowafundisha wananchi juu ya mbinu na mikakati ya kuanzisha, kuendesha na kuendeleza vyama vya ushirika.

Ndugu Mwenyekiti,

Katika mjadala wowote wa maendeleo unaohusu nchi changa na maskini kama yetu, huwezi kuepuka kutaja Ushirika. Umuhimu wa sekta ya Ushirika na Biashara ni mkubwa sana katika kuchangia maendeleo ya Taifa na kuondoa umaskini si katika nchi ya Tanzania tu bali kote duniani. Serikali za awamu zilizotangulia katika nchi yetu ziliutambua ushirika kama nyenzo muhimu ya wananchi ya kuunganisha nguvu na rasilimali zao ili kupambana na unyonge na hali duni ya kiuchumi.

Nchi yetu inayo historia ndefu ya ushirika. Ulianza kwenye miaka ya 1930. Ushirika ulianzishwa na wakulima kama chombo cha kuendeleza maslahi yao dhidi ya unyonyaji na ukandamizaji

wa mabepari na wakoloni. Ushirika uliendelea kukua kwa sababu mahitaji ya watu yalikua, na mazingira yaliendelea kubadilika.

Shughuli za kiuchumi zikianza kukua na kupanuka, lazima utaalamu na uendeshaji unaenda na wakati. Ni wazi kabisa kwamba mtu atahitaji kwa mfano, utaalamu wa utunzaji vitabu na kumbukumbu za mahesabu na biashara. Wadau pia wanahitaji utalaamu wa uongozi, utaalamu wa uuzaji na ununuzi, utaalamu wa ubunifu wa mifumo bora ya uendeshaji, na kadhalika. Na juu ya yote hayo, wanachama waliounda Ushirika watahitaji kuelimishwa ili waujue vizuri wajibu wao ili waweze kuulinda na kuudumisha. Ninafurahi na ninawapongeza kwa kuamua kuchukua majukumu haya ya msingi kwa maendeleo ya wakulima, wafugaji na wafanyabiashara wengine.

Ndugu Mwenyekiti,

Nimesema kuwa historia ya Ushirika nchini mwetu ni ndefu. Katika historia hiyo, ushirika siyo tu ulikuwa ukilinda na kuendeleza maslahi ya wakulima, bali ulitoa mchango muhimu katika harakati za kudai uhuru wa nchi yetu na hasa uhuru wa Tanzania Bara. Baadhi ya waasisi wa harakati za kupigania Uhuru wa nchi yetu, walitumia ushirika na vyama vya ushirika kama chombo cha kuhamasisha na kuandaa haki yao ya kujitawala. Ndani ya Ushirika walitoka baadhi ya viongozi waliokuwa mstari wa mbele kupigania uhuru. Hayati Mzee Paulo Bomani na Mzee George Kahama ni mfano mzuri wa wana-ushirika, viongpzi walioshiriki kidete katika harakati za kudai uhuru wa nchi yetu. Ndani ya Ushirika pia zilitoka fikra zilizosukuma mbele harakàti za ukombozi wa Taifa letu. Kuna wakati vyama vya Ushirika vilikuwa na nguvu kubwa sana kisiasa na kiuchumi. Vilimiliki rasilimali nyingi na kubwa. Vilikuwa kimbilio la wanyonge, hasa kwa ajili ya kupata masoko na pembejeo. Wananchi waliviamini vyama vyao vya Ushirika na waliona fahari ya kuwa wanachama. Katika historia ya maendeleo ya Taifa letu ni vigumu kusahau mchango wa ushirika. Huwezi basi kusahau Chuo cha Ushirika Moshi, mama wa Chuo hiki kipya tunachokizindua leo kwa kazi nzuri kilichofanya ya kufundisha Maafisa Ushirika na wana ushirika nchini.

Bahati mbaya sana, historia hiyo nzuri ya Ushirika nchini inaelekea kubakia kuwa kumbukumbu katika vitabu vya historia. Vyama vya Ushirika vingi vimekufa na vilivyopo viko katika hali mbaya. Kama ni wagonjwa basi wako chumba cha wagonjwa mahututi (ICU). Tatizo kubwa ni uongozi na uendeshaji mbovu. Vyama vingi vina madeni makubwa kwenye mabenki na kwa wakulima.

Kwa nyakati fulani fulani Serikali ililazimika kuyachukua madeni ya vyama vikuu vya ushirika ili kujaribu kuvinusuru vyama hivyo. Hizi zilikuwa ni juhudi za kuvifanya viweze kukopesheka ili viendelee kutoa huduma kwa wadau wake na kulipa madeni yao angalau kwa wakulima. Vipo vyama vingine vilivyonusurika kwa juhudi hizi, lakini kwa vingine haikuwezekana. Vimefilisika kabisa vikiwa havijatimiza wajibu wake wa kimsingi kwa wanachama wake.

Swali la msingi na muhimu kujiuliza hasa, ni nini kilichotokea mpaka tukafikia hali hii? Na, je tumejifunza nini juu ya kuzorota kwa ushirika nchini ? Naamini Chuo hiki kitatusaidia kupata majawabu

ya maswali haya. Nasubiri kwa hamu majibu hayo kwani nina dhamira ya kujaribu kufufua ushirika. Sina hakika kama nitafanikiwa. Katika juhudi hizo ningependa tusirudie tena makosa tuliyoyafanya huko nyuma. Naamini kwamba Chuo Kikuu hiki kipya kitakuwa ni sehemu muhimu ya juhudi za kufufua na kuendeleza Ushirika nchini mwetu.

Changamoto zetu, kwa pamoja, ni kwanza kabisa kuhakikisha kuwa tunapata viongozi wa ushirika ambao ni waadilifu na wanaowajibika kwa wanachama. Kadhalika tutafute mikakati na mbinu za kutumia, kuhimiza na kuhamasisha uanzishaji na uendelezaji wa Vyama vya Ushirika vyenye nguvu za kiuchumi na vinavyotumia mifumo ya kisasa ya biashara na menejimenti. Tunao pia wajibu kujenga mifumo imara na kuwa na sera muafaka za kifedha ambazo zitarahisha muingiliano katika utoaji wa huduma za kifedha kati ya Mabenki na Vyama vya Ushirika. Vilevile, tufanye juhudi za kuunganisha vyama vya mazao ya kilimo na makampuni ya kimataifa ya ununuzi wa mazao hayo. Ushirika wetu wa sasa unalo jukumu kubwa la kujenga wajasiriamali watakaoweza kumudu kasi ya sasa ya utandawazi na soko huria. Majawabu kwa changamoto hizi, na nyingine nyingi, ni muhimu katika kuhakikisha kwamba juhudi zetu za kuendeleza Ushirika zinatoa manufaa tunayoyatarajia.

Ndcgu Mwenyekiti, Waheshimiwa Viongozi na Wageni Waalikwa,

Serikali, kwa upande Wake, itaendelea kuchukua hatua mbalimbali kusidia kutatua matatizo yaliyokuwa yanavikabili Vyama vya Ushirika. Katika kufanya hayo, Serikali inategemea sana Chuo chetu hiki kwa ushauri. Nyie wenzetu ndio wenye utaalamu na uwezo mkubwa zaidi wa kusaidia. Kwa mfano, tutategemea sana utaalarnu wenu kwenye kutatua matatizo ya uongozi mbovu na uendeshaji usio makini. Pia tunategemea katika juhudi za kutatua matatizo ya elimu duni ya ushirika na ya kuendesha vyama kibiashara miongoni mwa wanachama na viongozi wao. Ninachotaka kusema hapa ni kwamba Serikali inakiona Chuo Kikuu cha Ushirika na Biashara kuwa mbia muhimu. Hivyo basi, tutatoa ushirikiano wake kwa Chuo hiki katika kutekeleza malengo yake kuhusu kuimarisha ushirika nchini.

Ndugu Mwenyekiti;

Katika miaka ya hivi karibuni kumekuwa na mwamko mkubwa, unaonitia moyo, miongoni mwa wananchi wa kuanzisha Vyama vya Ushirika vya Akiba na Mikopo - Savings and Credit Cooperative Societies - SACCOS. Uanzishaji na uendelezaji wa SACCOS unawapa wananchi fursa ya kupata huduma za kifedha, ambazo wengi wao wasingeweza kuzipata kwa kutumia taasisi nyingine za fedha.

SACCOS zimekuwa chanzo muhimu cha kuwapatia wananchi mikopo wanayoitumia kama mitaji kufanyia shughuli zao za kuwapatia kipato. Ningependa kuona ushirikiano baina ya SACCOS na Asasi nyingine za fedha na hasa Benki za Biashara unaimarishwa. Ushirikiano huo utatoa fursa kwa wananchi ya kupata mikopo kutoka Benki kwa masharti nafuu kupitia kwenye SACCOS zao mahali

walipo bila kulazimika kwenda Benki ya Biashara husika. Kubwa zaidi ni kwamba hizi SACCOS zinatusaidia kupunguza tatizo la ajira miongoni mwa wananchi. Tatizo la Ajira nimeliongelea sana wakati wa kampeni za Uchaguzi mwaka jana. Nafarijika sana kuona mwamko mkubvva wa kuanzisha SACCOS nchini, kwa kuwa natambua zitatusaidia sana kutimiza ahadi yetu kwa Watanzania ya kupunguza tatizo la Ajira nchini. Kwa kutambua manufaa haya, Serikali itaweka msukumo mkubwa katika kuwawezesha wananchi kuanzisha na kuendeleza SACCOS ili ziweze kuondoa tatizo la ukosefu wa mitaji ya kuendeshea shughuli zao. Natoa wito kwa wanataaluma ya Ushirika kuzisaidia SACCOS kwa mafunzo ya mbinu, mikakati na maarifa ya uendeshaji wake parnoja na utunzaji fedha na ujasiriamali.

Ndugu Mwenyekiti,

Naomba nitumie fursa hii kusisitiza dhamira ya Serikali ya Awamu ya Nne ya kutaka kuwawezesha Watanzania kiuchumi. Tayari tunayo nchini sera ya uwezeshaji iliyotayarishwa na Serikali ya awamu ya Tatu, Nimeliweka jukumu la Uwezeshaji kama jukumu mahsusi la Wizara ya Mipango, Uchumi na Uwezeshaji. Lakini jukumu hilo la Serikali litakuwa rahisi kulitekeleza pale tu wananchi watakapoungana katika vikundi, kwa maneno mengine, katika Ushirika. Kwenye hotuba yangu ya Bunge Desemba mwaka jana nilitoa ahadi na changamoto kwa vikundi mbalimbali, vya wafugaji, wakulima, wavuvi, mafundi waashi, n.k. kuungana ili iwe rahisi kwa Serikali kuwawezesha. Vilevile, nilitoa changamoto kwa wasomi nao kuungana katika makundi ya taalurna zao.

Ndugu Mwenyekiti;

Kwa kuwa leo tuko kwenye taasisi ya Elimu ya Juu, tena ya elimu ya juu kabisa kuhusu Ushirika, nadhani ni mahali muafaka kurudia tena ile ahadi na changamoto yangu. Ninawashauri wasomi wa fani na taaluma mbalîmbali kama vile kilimo, mifugo, uvuvi, uhandisi, usanifu wa majengo, sheria, uhasibu na kadhalika kuungana na kuanzisha shughuli za kiuchumi kutumia taaluma zao. Niliahidi kuwa, nitajitahidi kuwasaidia kwa hali na mali katika shughuli zao. Tafadhali jitokezeni.

Katika dunia ya utandawazi na ushindani unaoambatana nao, Watanzania wasomi watabaki nje ya mkondo iwapo hawatakuwa wabunifu zaidi, mkaungana na kuanzisha ushirika au kampuni za shughuli za taaluma zenu. Lakini mkiamua kuungana na kuanzisha ushirika na makampuni yanaoendeshwa kwa misingi halisi ya kibiashara, Serikali, kupitia vyama vya taaluma zenu, itawaunga mkono, itawasaidia na itawawezesha. Serikali inakaribisha mawazo kutoka kwa vyama vya kitaaluma pamoja na chuo hiki, juu ya namna bora ya kufikia lengo hilo. Ningependa wasomi wetu muwe kiini cha kujenga kada ya wajasiriamali wasomi na wazalendo hapa nchini. Ningependa Ushirika wa wasomi uwe mfano wa uendeshaji wa Ushirika wa nyanja nyingine kwa ufanisi.

Ndugu Mwenyekiti,

Nimefurahi kusikia kwamba Chuo hiki kipya, kimejiandaa kuzikabili changamoto za utandawazi. Tunafahamu kwamba ushindani katika soko unachochewa na utandawazi hivyo, kujiendeleza hadi kiwango cha juu cha elimu ni muhimu kwani inawawezesha wananchi na vikundi kubuni mbinu za kisasa za ushindani katika soko huria. Hatua ya kujiendeleza ndiyo itakayowezesha ujenzi wa uchumi vikundi (associative economy).

Kwa watu walio maskini, hakuna njia mbadala ya kujikomboa zaidi ya njia ya uchumi vikundi. Uchumi vikundi ndio pekee unaoweza kuwashirikisha wananchi walio wengi hapa nchini katika harakati za kuondokana na umaskini. Natoa rai kwa Chuo hiki kuendelea kuwandaa vijana wa mijini na vijijini kujifunza namna ya kuunda na kuendesha uchumi vikundi ili waweze kuukabili uchumi wa ushindani na kuondoa umaskini kwa kutumia nguvu ya ushirika. Utajiri wa taaluma hii mnao na nawaomba muendelee kuutumia kwa manufaa na maendeleo ya Taifa letu. Ni matumaini yangu, kwamba wadau wote wa ushirika na biashara; wazazi, wawakilishi wa mashirika, vikundi mbalimbali na Watanzania kwa ujumla watakifanya Chuo hiki kipya kuwa hazina ya maarifa na ujuzi wa hali ya juu kuhusu ushirika na biashara.

Ndugu Mwenyekiti,

Ni mategemeo yangu pia, kuwa masomo yatakayofundishwa hapa Chuoni yatakidhi mahitaji ya wadau na kuwa jibu halisi la changamoto za maendeleo. Ndio maana basi, nimefurahi sana kusikia kwenye taarifa yenu kwamba katika moja ya mambo mnayofundisha ni kozi maalum ya kuongeza uwezo wa usimamizi wa miradi ya kitaifa na kimataifa kwa watendaji wa halmashauri za wilaya. Mkifanya hili mtakuwa mmelisaidia Taifa letu kwa namna ya kipekee.

Şuala la kujenga uwezo wa usimamizi na utendaji kwa Serikali za Mitaa ni jambo linaloniumiza sana kichwa. Halmashauri ya Wilaya au Miji ndicho chombo muhimu cha mamlaka ya umma nchini. Matazamio haya hayafikiwi kwa sababu ya ujuzi na uwezo mdogo wa usimamizi wa Halmashauri hizo kwa upande wa Madiwani. Madiwani ndicho kielelezo na mwakilishi wa umma katika kutumia mamlaka yao. Ni matumaini yangu kuwa mafunzo hayo yataanza mapema iwezekanavyo na mamlaka zinazohusika zitayachangamkia.

Ndugu Mwenyekiti,

Uzinduzi wa Chuo Kikuu cha Ushirika ni kurasimisha ongezeko la Vyuo Vikuu hapa nchini. Kitendo hicho kinaongeza uwezo wa nchi wa kutoa elimu ya juu kwa wananchi wake. Elimu ya juu itokayo hapa haina budi iwawezeshe wahitimu kuwa na uelewa mpana zaidi wa mahitaji ya jamii wanamoishi. Pia, iwawezeshe washiriki kvva vitendo katika jitihada za kukidhi mahitaji hayo. La muhimu zaidi ni kwamba elimu itolewayo hapa iwe elimu bora na ya kiwango kinachokubalika nchini na kimataifa. Katika elimu ya juu hakuna digrii ya nchi fulani tu. Digrii huwa zina sifa na heshima ya kimataifa.

Changamoto kwa vyuo vyote vya elimu ya juu ni kuhakikisha kuwa mafunzo yatolewayo sasa na yatakayoanzishwa baadaye, yanalenga kuleta matokeo chanya kwa maisha ya Watanzania. Kila mara mtakapobuni mitaala mipya, lazima kujiuliza ni kwa kiasi gani mhitimu wa mitaala hiyo atasaidia wananchi katika kuondokana na kero zao na kuboresha hali yao ya maisha. Kwra hiyo programu za mafunzo zizingatie mahitaji halisi ya Watanzania. Mahitaji namba moja kabisa ni kuondokana na urnaskini. Hivyo, elimu ya chuo kikuu nchini iwawezeshe wahitimu wake kutoa mchango wa kuwawezesha Watanzania kupunguza na hatimaye kuondokana na urnaskini.

Ndugu Mwenyekiti

Mwisho, napenda kuchukua fursa hii kushukuru watu na mashirika mbalimbali kwa kusaidia katika kazi hii kubwa. Nalishukuru pia Baraza la Chuo Kikuu cha Kilimo Sokoine kwa kuwa mlezi makini wa chuo hiki mpaka hapo kitakapoweza kusimama chenyewe kama Chuo Kikuu. Vilevile, nalipongeza Baraza la Uongozi wa Chuo cha zamani cha Ushirika kwa kazi kubwa waliyoifanya katika kusimamia chuo hadi kufikia kupanda hadhi na kuwa chuo kikuu.

Aidha, nawashukuru na kuwapongeza wakufunzi na wafanyakazi wote wa chuo kwa mchango wao katika mchakato wa mabadiliko ya chuo.

Ahadi yangu kwa chuo hiki kipya ni kwamba Serikali itaendelea kukisaidia kulingana na Sera ya Elimu ya Juu na uwezo wake wa kiuchumi. Napenda vile vile kuchukua nafasi hii kuzishukuru nchi wahisani kwa mchango wao kwa maendeleo ya Chuo hiki tangu kianze mpaka sasa.

Ndugu Mwenyekiti; Wageni Waalikwa, Mabibi na Mabwana;

Kwa heshima na taadhima sasa ninatangaza kwamba Chuo Kikuu Kishiriki cha Ushirika na Stadi za Biashara cha Moshi, kimezinduliwa rasmi.

Ahsanteni sana kwa kunisikilizi.